**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salaam***
***22 Julai, 2026***

## YAH: UTEUZI NA UHAMISHO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi na uhamisho wa viongozi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, uteuzi na uhamisho huo ni kama ifuatavyo:

(i) Dkt. Latifa Mohammed Khamis ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano. Kabla ya uteuzi huu, Dkt. Khamis alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE);

(ii) Bi. Prisca Burton Lwangili ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kabla ya uteuzi huu, Bi. Lwangili alikuwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI;

(iii) Bw. Abdallah Hassan Mitawi amehamishwa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi;

(iv) Balozi Baraka Haran Luvanda amehamishwa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria;

(v) Dkt. Franklin Jasson Rwezimula amehamishwa kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;



*Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

(vi) Dkt. Maduhu Isaac Kazi amehamishwa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwenda kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Mazingira; na

(vii) Bw. Ephraim Balozi Mafuru ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE). Kabla ya uteuzi huu, Bw. Mafuru alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Aidha, uapisho wa Naibu Makatibu Wakuu wateule utafanyika kwa tarehe itakayopangwa baadaye.

Shaaban Kissu
Kny. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu